




Je, kwa nini Hepatitisi B
ni muhimu kwangu?

Kwa sababu...

Hepatitisi B ni mojawapo kati ya maambukizo yanayotokea sana ulimwenguni.

Hepatitisi B hutokea zaidi mionganini mwa watu waliozaliwa barani Afrika na sehemu zingine ulimwenguni.

Kwenye jamii za Kiafrika nchini Marekani, baina ya 5% na 18% ya watu wana hepatitisi B.




Kwa sababu...

Hepatitisi B ni mojawapo kati ya maambukizo yanayotokea sana ulimwenguni.

Hepatitisi B hutokea zaidi miongoni mwa watu waliozaliwa barani Afrika na sehemu zingine ulimwenguni.

Kwenye jamii za Kiafrika nchini Marekani, baina ya 5% na 18% ya watu wana hepatitis B.



Je, Hepatitisi B ni nini?



Hepatitisi B ni uambukizo
mkali unaoweza kusababisha
ugonjwa mkali wa ini na hat
saratani ya ini.

Kudumisha afya ya ini lako ni muhimu kwa sababu
ini lina kazi nyingi kwenye mwili wako.


Linameng'anya chakula.



Linawastanisha nishati.




Linajenga misuli.




Linavunjavunja sumu.

Linapambana na maambukizo.

Linasindika dawa.




Linahifadhi vitaminii.



Linasaidia kukausha damu.

Mtu hawezi kuishi bila
ini lake!



Hepatitisi B

*Kufahamu Hepatitisi B na Kukuza Vipimo
Miongoni mwa Jamii za Wahamiaji wa Kiafrika*



Mwongozo kwa wafanyakazi wa afya ya jamii, wakufunzi wa afya, watoa huduma wa uangalizi wa afya na wataalamu wengine




U.S. Department of
Health and Human Services
Centers for Disease
Control and Prevention



Habari njema:

Inaposhughulikiwa na daktari, hepatitis
B ni maradhi ambayo watu wanaweza
kuishi nayo kwa muda mrefu.

Kwa kuchunga afya yao, watu
wanaweza kuishi maisha
marefu na yenye manufaa.



Unaweza kusaidia
kudumisha afya ya jamii
kwa kujifunza kuhusu
hepatitisi B na kukuza
ufahamu na vipimo.


Misingi ya Hepatitisi B



Hepatitisi B ni mojawapo kati ya maambukizo yanayotokea sana ulimwenguni.

Ulimwenguni

Zaidi ya watu milioni 250 wanaishi na hepatitisi B



Nchini Marekani

Karibu watu milioni 1 wana maambukizo ya hepatitisi B

Watu wengi wenye hepatitis B hawajui kuwa wameambukizwa!



Kuna aina 2 za maambukizo ya hepatitis B.

Hafifu



Uambukizo wa muda
mfupi

Kali




Uambukizo wa maisha
yako yote

Umri ambapo mtu anaambukizwa unang'amua aina ya uambukizo atakaokuwa nao.

Hafifu

Uambukizo unaodumu kwa chini ya miezi 6



- Hautokei sana
- Mara nyingi hutokea kwa kuambukizwa unapokuwa mtu mzima
- Unaondoka mwilini ndani ya miezi 6

Kali

Uambukizo unaodumu kwa maisha yako yote



- Hutokeea sana
- Mara nyingi hutokea kwa kuambukizwa utotonii
- Hudumu kwa maisha yako yote



Ingawa hepatitis B inaweza kuzuiwa
kwa chanjo wakati wa kuzaliwa, si
watoto wote wachanga wanaopokea
chanjo hiyo.

Wanawake wengi wajawazito hawajui
kama wameambukizwa, na bila kujua
wanawaambukiza watoto wao
wachanga na virusi hivyo.

Bila chanjo, wengi kati ya watoto hao
wachanga watapata maambukizo
makali, ya muda mrefu.

Mtu pia anaweza kupata hepatitis B kuitia:



Damu

Kugusisha damu kwa damu na mtu
aliyeambukizwa




Mama hadi kwa
mtoto wakati wa
kuzaliwa



Kugusisha vyombo
Kushiriki zana za usafi
(vijembe, miswaki, vipuli
n.k.)



Chale, vitobolewa mapambo,
vinyozi, kukwaruzisha, na
utendakazi wa kutahiri bila
kutakasa vyombo



Kugusa
kwenye
uangalizi
wa afya



Kushiriki
sindano

Ngonon

Kugusana moja kwa moja na
viowevu vya kingono vya mtu
aliyeambukizwa




Ngono bila Kinga

Kuna hatari wakati wa aina
yooyote ya kugusana kingono

Hepatitis B KATU haisambazwi kwa:

Chakula

Au kula chakula pamoja na mtu
aliyeambukizwa




Maji

Kunywa kutoka kwenye kikombe cha
mtu aliyeambukizwa au kushiriki
choo pamoja



Kumchemulia
au kumkoholea
mtu



Kugusana



Kukumbatiana



Kunyonyesha




Kubusiana



Chini ya asilimia 10% ya watu walioambukizwa na hepatitis B kali wana dalili.

Ikiwa dalili zitajitokeza kwenye hepatitis B kali, huenda ikawa ni ishara ya maradhi ya ini ya muda mrefu:



Macho au ngozi manjano, maumivu tumboni, kutapika, kuhisi uchovu, kuumwa na viungo, mkojo wenyе rangi nzito au kinyesi chenye rangi ya udongo

-  Ingawa hepatitisi B hutokea sana barani Afrika, watu hawajui kuwa wao wameambukizwa.
-  Watu wanaweza kuhofia kupimwa. Huenda ikawa wanaamini visivyo kuwa wangepata dalili ingekuwa wana maradhi, au wanashikilia mambo ya uongo au hawawezi kufikia uangalizi wa afya.
-  Kutojua kuhusu uambukizo ni hatari kwa afya.
-  Bila uangalizi wa afya wa mara kwa mara na uwezekano wa matibabu, mtu mwenye hepatitisi B anakumbana na hatari iliyooongezeka ya kufariki mapema au kuwaambukiza wengine bila kujua.

Kipimo cha hepatitis B ni kipimo rahisi cha damu.

Kinaweza kufanywa na daktari wa familia, mtaalamu wa ini au kwenye kongamano la afya la jamii.



Ni upesi na rahisi na matokeo yatapatikana kwenye siku chache.

Baada ya mtu kupimwa:

Ikiwa matokeo ya kipimo
yanaonyesha kuwa



Mtu KATU hajaambukizwa

- Anafaa kupewa chanjo ili kuzuia asipate hepatitis B

Mtu amembukizwa

- Anafaa kuonana na daktari ili kufanyiwa vipimo vya ziada
- Ahakikishe kuwa wanafamilia na washiriki wake wa kingono wamepimwa



Mtu anayepimwa na kupatikana kuwa ana hepatitis B anaweza kudumisha afya kwa:

1

Kuonana na daktari wake mara 1-2
kwa mwaka.

- Mwafaka zaidi awe daktari mwenye uzoefu wa kushughulikia hepatitis B
- Daktari atamfanyia vipimo vya ziada, na ikihitajika, atapendekeza matibabu




2

Kuishi mtindo wa maisha
unaodumisha afya

- Kula chakula chenye lishe bora
- Kuendelea kuushughulisha mwili
- Kuepuka sigara na pombe

Hizi zina sumu zinazoweza kudhuru ini



Hepatitisi B kali haina tiba.

Madai kuwa dawa au tiba za mitishamba
zinaweza kutibu virusi hivi ni ya uongo.



Kuna matibabu ya hepatitis B.

Lakini, habari njema ni kuwa...

*Kuna matibabu yanayoitwa
kingavirusi, yanayoweza kuvihibiti
virusi kwa ufanisi na kuzuia
kuharibika kwa ini.*



Je, kwa nini watu wapimwe ili kugundua kama wana hepatitis B?



Hepatitis B inaweza kushughulikiwa na kutibiwa!



Mtu hafai kungojea mpaka awe mgonjwa.



Watu wengi huwa hawana dalili.



Wanafaa kupimwa sasa!



Kuna chanjo salama na yenye ufanisi ambayo inaweza kuwalinda unaowapenda ambao hawana hepatitis B.

Kupimwa sasa kunaweza kumruhusu mtu adumishe afya kwa ajili ya nafsi yake mwenyewe na kwa ajili ya anaowapenda!





Una nguvu ya kuokoa maisha kwa:

- Kuelimisha kuhusu hepatitis B
- Kukuza vipimo kwenye jamii yako





Kuongea kuhusu hepatitis B kwa njia inayozingatia tamaduni kunaweza kukupatia changamoto.



Kujua dhana potofu na jinsi ya kuzidhoofisha kunaweza kusaidia kuangamiza unyanyapaa na kufikisha maelezo sahihi.



Dhana Potofu ya #1: Dalili



Sina dalili zozote.
Je, bado ninaweza
kuwa na hepatitis B?



Ndio.
Watu wengi wenye
hepatitis B
hawana dalili zozote!

Ukweli wa #1

Watu wengi wenye hepatitis B hawana dalili zozote.

Kumbuka:

Watu huenda wakawa wamezoea kutibu magonjwa tu wanapokuwa na dalili. Watu huenda wakawa hawahisi dharura ya kupimwa.

Vidokezo Muhimu:


- Wajulishe wanajamii kuwa watu wengi wenye hepatitis B mara nyingi huwa hawana dalili, ingawa hata maini yao yanaweza kuwa yameharibika.
- Wakumbushe watu kuwa wana nguvu ya kuboresha afya zao sasa, ili kuzuia matatizo mazito ya ini kwenye siku za usoni.
- Kipimo cha hepatitis B ni kipimo rahisi cha damu. Ni njia pekee ya kujua kama mtu ameambukizwa na maradhi haya!



Dhana Potofu ya #2: Usambazaji



Sijafanya chochote
cha kunitia kwenye
hatari ya kuambukizwa
hepatitisi B.
Je, bado ninaweza
kuwa nayo?



Ndio.
Watu wengi
wanaambukizwa hepatitisi
B wanapokuwa watoto
wachanga au watoto
wadogo.

Ukweli wa #2


Watu wengi wanaoishi na hepatitisi B waliambukizwa wakati wa kuzaliwa au walipokuwa watoto wadogo.

Kumbuka:

Baadhi ya watu wanahuisha hepatitisi B na tabia za kujihatarisha na zisizodumisha afya. Watu huenda ikawa hawajui kuhusu jinsi watu wengi wanavyoambukizwa.

Vidokezo Muhimu:



- Sisitiza njia inayotokea sana ya kusambaza hepatitisi B; ambayo ni kupitia kugusana kwa damu wakati wa kuzaliwa au wakati wa utotoni.
- Kuwakumbusha kuwa hepatitisi B ni mojawapo kati ya maambukizo yanayotokea sana ulimwenguni kunaweza kukusaidia kufanya kupimwa kuwe jambo la kawaida.



Dhana Potofu ya #3: Uangalizi wa Kimatibabu



Je, kuna tiba za
hepatitisi B?



Ndio.
Tiba zinapatikana
ambazo zinaweza
kuwasaidia watu
wadumishe afya zao.

Ukweli wa #3

Tiba zinapatikana ambazo zinaweza kuwasaidia watu wadumishe afya zao.



Kumbuka:

Watu huenda ikawa wana wasiwasi kuwa kupimwa na kupatikana kuwa wana hepatitis B kutababilisha maisha yao yote –lakini si lazima iwe hivyo!

Vidokezo Muhimu:


- Watu wenyewe hepatitis B bado wanaweza kuisha maisha marefu, yenye afya na yenye manufaa.
- Hepatitis B mara nyingi husonga polepole. Hatari kubwa kabisa ni kutojua kuwa mtu amembukizwa!
- Hepatitis B inaweza kushughulikiwa kwa ufanisi kwa muda kwa kuonana na daktari na kutumia matibabu ikihitajika.



Fahamu:


Hakuwezi kuwa na unyanyapaa wala
hofu unaohusishwa na hepatitis B.

Tujifahamishe kuhusu jinsi ya kuvunja
vizuizi hivi wakati wa kuelimisha.



Kuangamiza Unyanyapaa: Maelezo Potofu

Unyanyapaa unaweza kutokana na maelezo potofu



Maelezo potofu yanaweza kuibua nadharia kuhusu jinsi mtu alivyopata virusi.


Watu wanaweza kuchukulia kuwa mtu ameambukizwa hepatitis B kupitia:

- Tabia zisizokuwa na maadili
- Matumizi ya dawa za kulevyta
- Kuwa na washiriki wengi wa kingono



Kuangamiza Unyanyapaa: Maelezo Potofu

*Ili kudhoofisha maelezo potofu,
sisitiza ukweli!*




Watu mara nydingi wanapata hepatitis B
kutoka:

- Kwa mama zao wakati wa kuzaliwa
- Kwa mgusano na damu wanapokuwa watoto wadogo

Mtu yoyote anaweza kuyapata maradhi haya bila kujali maadili yao ya kidini au kitamaduni



Kuangamiza Unyanyapaa: Hofu




Unyanyapaa pia unaweza kuibuka kutokana na hofu.

- Kuonekana unapimwa
- Kuushughulikia uambukizo wa hepatitis B
 - Gharama
 - Kuonana na daktari mara kwa mara
 - Uzito kwa familia
- Unyanyapaa wa kijamii
 - Kutengwa na marafiki na familia
 - Kulaumiwa na jamii

Kuangamiza Unyanyapaa: Hofu



Ili kuangamiza hofu, kufanye kupimwa hepatitis B kuwe kama kawaida na sisitiza nyenzo zipatikanazo.



- Nyenzo zinapatikana ili kuwasaidia watu wanaoishi na hepatitis B.
- Hepatitis B ni virusi vinavyotokea sana na vinaweza kushughulikiwa kwa ufanisi kwa kuonana na daktari na kufanya mabadiliko rahisi kwenye mtindo wa maisha.
- Kila jamii inapojua maelezo sahihi zaidi, ndipo unyanyapaa utapungua kuhusiana na hepatitis B!


**Wewe una kazi muhimu kwenye jamii yako,
na una nguvu ya kukuza ufahamu na vipimo vyat hepatitis B!**



Vidokezo muhimu:

- ▶ Usiwahi kupuuza wasiwasi wa mtu mwingine. Daima himiza wanajamii wajihisi wana nguvu na washughulike kuhusu afya zao, ili waweze kudumisha afya zao kwa ajili yao binafsi na kwa ajili ya familia zao.
- ▶ Mtu akipimwa na akipatikana kuwa ana hepatitis B, kuna nyenzo nyingi zipatikanazo za kuwasaidia washughulikie uambukizo huo, hata kama hawana bima ya afya.
- ▶ Ubainishi wa kuwepo kwa hepatitis B si kifungo cha kifo, na kwa kuishi mtindo wa maisha unaodumisha afya na kufuatilia kwa daktari, watu wanaweza kuishi maisha marefu na yenye manufaa!

Huko peke yako! Hizi hapa nyenzo zinazopatikana ili kukusaidia:



Je, ninaweza kuwapata wapi madaktari ili kuangaliwa na kupimwa?

Saraka ya Wataalamu wa Ini ya Taasisi ya Hepatitis B
www.hepb.org/physiciandirectory

Kitafuta Kituo cha Afya Kilichoidhinishwa Kishirikisho (FQHC)
www.findahealthcenter.hrsa.gov

Je, ninaweza kuyapata wapi maelezo zaidi kuhusu hepatitis B?

► Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Maradhi (CDC)

- Maelezo ya kimsingi kuhusu hepatitis B, miongozo na PDF zinazopakulika
- Nyaraka za ukweli zinazochapishika, video za PSA, grafiki za maelezo, maswali ya majaribio, na zaidi kwa lugha kadhaa
- Mabango ya bure

www.cdc.gov/knowhepatitisB

► Taasisi ya Hepatitis B

- Baruapepe na simu za dharura
- Maelezo bainifu
- Nyaraka za ukweli zinazochapishika
- Video za kuhamasisha

www.hepb.org

Kuna njia nyingi za kujumuisha elimu ya hepatitis B kwenye jamii yako.

Ongea na wanajamii kuhusu
afya na hatari yao
kuhusiana na hepatitis B.



Kuwa mwenyeji wa kipindi
cha elimu, kongamano la
afya au tukio la vipimo vya
hepatitis B.



Kuza kongamano la afya
la eneo hilo ambalo
linafanya vipimo vya
hepatitis B.

Onyesha maelezo ya
ukweli, brosha, na
mabango ya kielimu.



Shiriki machapisho ya CDC
na Taasisi ya Hepatitis B
kwenye mitandao ya kijamii.

Furushi la zana
linajumuisha maelezo na
usaidizi zaidi wa kuyaleta
pamoja mawazo haya.

Asante kwa kusaidia kusambaza maelezo kuhusu
hepatitisi B!



Baada ya kutazama onyesho hili, tafadhalii
kamilisha tathmini-binafsi fupi.

Bofya Hapa!

Maoni yako yanaweza kutusaidia tukupatie
nyenzo zitakazokusaidia zaidi!

Ikiwa una maswali au unahitaji usaidizi wa ziada, tuma
baruapepe kwa: info@hepb.org



U.S. Department of
Health and Human Services
Centers for Disease
Control and Prevention

